

TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA (TACAIDS)



**TAARIFA YA UFUATILIAJI
NA TATHMINI YA UKIMWI
MKOA WA KIGOMA**

OKTOBA, 2007

ISBN 978-9987-519-18-7

Yaliyomo

Ufafanuzi wa Majedwali	v
Vifupisho	vi
Shukrani	vii
Muhtasari	viii

Sura ya 1 Utangulizi **1**

1.0 Historia	2
1.1 Wasaa wa mkoa	2
1.2 Malengo ya kitaifa ya kudhibiti Ukimwi	2
1.3 Malengo ya safari	2
1.4 Uratibu uliotumika katika kupata taarifa	2
1.5 Makundi yaliyohusika katika usaili/majadiliano	3

Sura ya 2 Hali ya VVU/UKIMWI **4**

2.0 Maambukizi ya VVU/UKIMWI	4
2.1 Ukubwa wa tatizo	5
2.2 Ufahamu wa VVU/UKIMWI mkoani.	5

Sura ya 3 Matokeo ya Usaili **7**

3.0 Yaliyopatikana kwenye usaili wa makundi mbalimbali.	7
3.1 Matatizo yanayowakabili katika maisha yao.	8
3.2 Njia kuu za maambukizi	8
3.3 Vichochezi vya maambukizi	9
3.4 Maoni/Mapendekezo	10
3.5 Nini kifanyike kupunguza maambukizi	16
3.6 Vikwazo vya kupima UKIMWI	17
3.7 Madhara yanayotokana na UKIMWI	17

Sura ya 4 Uratibu katika Mkoa **18**

4.0 Uratibu katika ngazi ya mkoa	18
4.1 Idara za Halmashauri	19
4.2 Idara za afya	20
4.3 Usambazaji wa Kondomu	21
4.4 Huduma za Upimaji wa Hiari na Ushauri Nasaha	21
4.5 Huduma ya Utoaji damu salama.	22

4.6 Huduma ya maambukizi ya kutoka mama mjamzito kwenda kwa mtoto, PMTCT	23
4.7 Huduma za utoaji wa Dawa za Kufubaza (ARV)	24
4.8 Wadau wa UKIMWI mkoani Kigoma.	24
4.9 Wakala wa TACAIDS Mkoani Kigoma	25
4.10 Changamoto katika Uratibu	27

Sura ya 5 Changamoto na Mapendekezo **28**

5.0 Changamoto na matatizo	28
5.1 Mapendekezo	28

Sura ya 6 Hitimisho **30**

Hitimisho.	30
------------	----

Sura ya 7 Viambatisho **33**

7.0: Takwimu za mkoa wa Kigoma	33
7.1: Majina ya Watendaji	34
7.2: Taarifa Mbalimbali	35
7.3: Programu ya ziara mkoani Kigoma	36

Faharasa **37**

UFAFANUZI WA MAJEDWALI

Sura ya 1: Utangulizi

Jedwali 1: Utawala	2
--------------------	---

Sura ya 2: Hali ya VVU/UKIMWI

Jedwali 2(a): Hali ya maambukizi kwa asilimia	4
Jedwali 2(b): Taarifa za magonjwa ya ngono mwaka 2006	4

Sura ya 4: Uratibu katika Mkoa

Jedwali 4(a) Ushauri nasaha na Upimaji wa hiari, VCT, 2005	24
Jedwali 4(b) Ushauri nasaha na Upimaji wa Hiari, VCT, 2006	24
Jedwali 4(b(i)) Maendeleo ya Kampeni ya Upimaji Mkoani Kigoma	25
Jedwali 4(c) Hali ya maambukizo kwa wanaojitolea Damu ,2005	25
Jedwali 4(d) Hali ya maambukizo kwa wanaojitolea damu ,2006	25
Jedwali 4(e) Maambukizi ya VVU toka kwa mama mjamzito kwenda kwa mtoto,2005	26
Jedwali 4(f) Maambukizi ya VVU toka kwa mama mjamzito kwenda kwa motto.2006	26
Jedwali 4(g) Mchanganuo wa asasi zinazojishughulisha na UKIMWI mkoani	27
Jedwali 4(h) Mchanganuo wa asasi zilizopatiwa ruzuku ya mfuko wa CARF	28
Jedwali 4(i) Mchanganuo wa mfuko wa CARF kwa maeneo dhamiriwa	28

VIFUPISHO

- UKIMWI Upungufu wa kinga mwilini.
- ARV Dawa za Kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi.
- BAKWATA Baraza la kuu la Waislamu Tanzania.
- JKT Jeshi la Kujenga Taifa
- HBC Huduma za Nyumbani.
- VVU Virusi Vya UKIMWI.
- PMTCT Uzuiaji wa Maambukizi kutoka mama mjamzito kwenda kwa mtoto
- RC Mkuu wa Mkoa
- RMO Daktari mkuu wa Mkoa
- WAVIU Wanaoishi na virusi vya UKIMWI.
- RS Sekretarieti ya Mkoa.
- NACP Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI.
- GLOBAL FUND Mfuko wa Dunia.

SHUKRANI

Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) inapenda kutanguliza shukurani zake za dhati kwa wadau wote na watekelezaji wote wa masuala ya Ukimwi mkoani Kigoma.

Shukurani za pekee ziwaendee makamishna wa TACAIDS, Mh, Calista Simbakalia na Mh. Joan Chamungu kwa msaada na mchango wao katika kudhibiti gonjwa la UKIMWI.

Shukurani za wazi ziwaendee pia, Wakala wa TACAIDS mkoani Kigoma (CARE International) Bw. Joseph Fungo, vilevile Bw. Emmanuel Ndaki, Bi. Angela Jonathan (CHAC), Bibi Zilpa Kisonzela (RACH) pamoja na Bw. Hassan Mrage (DACC).


Tume inapenda pia Kuwashukuru Bw.Vitalis Makayula na Bi. Joan Chamungu Kutoka NACOPHA kwa msaada wao wakati wa ziara hii mkoani Kigoma.

Shukurani zinamuendea pia Dr. Mgosha kwa msaada na ushauri wake wa Kitaalamu kuhusiana na mambo mbalimbali mkoani hapo.

Vilevile tunapenda kushukuru mchango wa wakuu na watendaji wa mkoa wa Kigoma pamoja na Daktari wa Mkoa Anatolia Yaba, kwa sababu bila ya mchango wao ripoti hii isingewezekana.

Vilevile Tume inapenda kuwashukuru sana maofisa wake pamoja na waandishi wa habari na wakuu wa wilaya za Kigoma, makundi mbalimbali kama vile NACOPHA, WAVIU, KIVIDEA kwa msaada na mchango wao mkubwa.

Shukurani za pekee zinawaendea wakazi wa Kigoma kwa wepesi wao wa kujifunza na uwazi wao wa kujadili na kutoa maoni kuhusiana na masuala ya kimkoa, kitaifa na kimataifa katika kukabiliana na kuzuia maambukizi ya magonjwa ya zinaa na VVU/UKIMWI, ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha ripoti hii.



Fatma Mrisho
Mwenyekiti Mtendaji

MUHTASARI

Ikiwa na kiwango cha asilimia 7 cha ushamiri katika kundi la watu wazima, VVU ni tatizo kubwa sana kwa afya ya jamii ikiwa nyuma ya Malaria kwa kuwa tishio kwa jamii. Inaathiri sana afya na maendeleo ya jamii na uchumi-ikipunguza kiwango cha maisha ,inaongeza umaskini na kuchochea upungufu wa chakula/lishe (Mpango wa taifa wa Kudhibiti UKIMWI,NACP-2003).

Ripoti hii ilitayarishwa kutokana na haja ya kupitia hali ya UKIMWI nchini, Inatoa muhtasari na uelekeo wa VVU/UKIMWI mkoani Kigoma.

Ziara mbalimbali zilifanyika katika mikoa mbalimbali ,Kigoma ikiwemo ili kuangalia ukubwa wa VVU/UKIMWI nchini.

Malengo ya ziara yalikuwa ni:

- Kuangalia na kutathmini hali halisi ya UKIMWI mkoa wa Kigoma.
- Kukutana na wadau mbali mbali ili kubaini na kupata maoni yao kuhusu hali, vichocheo ,yanayotendeka pamoja na ushauri wao kuhusu mwitikio wa kudhibiti UKIMWI.
- Kushauriana kuhusu njia wanazooona zinafaa kutatua matatizo yanayohusu UKIMWI.
- Kutoa ushauri wa kitaalam unaohusu masuala ya UKIMWI.
- Kuwezesha NACOPHA kuunda Baraza kwenye ngazi ya Halmashauri.

Timu ya ziara ya Kigoma ilishirikisha maofisa wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), makamishna wa Tume, maofisa wa wizara ya afya na wabia wa maendeleo.

Mbinu iliyotumika katika mahojiano ulikuwa ni shirikishi ambapo wenyeji walihojiwa na kupewa maswali ya kujibu.

Ziara hiyo ilibaini yafuatayo:

- Hali imeonesha kuwa janga la ugonjwa wa UKIMWI limebaki kama lilivyokuwa miaka 24 iliyopita. Kama kuna mabadiliko basi ushahidi mwingi unaonesha kuwa ni mabadiliko ya kuongezeka maambukizi kati ya Watanzania.
- Mapitio yameonesha kuwa yawezekana kuna mambo ambayo ama hayatekelezwi ipasavyo na vyombo husika au shughuli zote za mapambano dhidi ya ugonjwa huu ziko nje ya mstari kwa maana kuwa kuna makosa katika mipango na utekelezaji wa mapambano dhidi ya UKIMWI.

Ni maoni ya wengi kuwa kiwango cha maambukizi ni zaidi ya asilimia 2 iliyobainishwa na **THIS** (2004). Hii ni kwa sababu ya ongezeko la tabia hatarishi kama vile ongezeko la madanguro na nyumba za kulala wageni,masoko ya jioni, wasichana kujiuza na kadhalika.

Ugawaji wa dawa za kupunguza makali ya virusi (ARV) ulianza mwaka 2006 katika hospitali ya mkoa, si chini ya vituo saba (7) vinavyotoa huduma hii bure.

Hakuna ripoti ya idadi kamili ya watoto yatima hapo mkoani.

Mashine za CD4 bado ni tatizo mkoani na tatizo huwa ni uchache wa mashine au mashine huwa ni mbovu.

Kondomu zinaleta changamoto kubwa sana:

- Idadi kubwa ya watu hawajui jinsi ya kuzitumia.
- Kondomu za kike ni chache.
- Ugawaji wa kondomu mkoani haujafikia walengwa wote mkoani, na kondomu zilizosambazwa ni chache.
- Watu wanaogopa kununua kondomu kwa sababu wanaogopa kuonekana wazinifu. Hii imesababisha kondomu nyingi kuuzwa kwa siri.

Kuna malalamiko mengi ya upungufu wa wanasih katika vituo vya ushauri nasaha na kupima, na vituo vingine hufungwa siku zote. Wanasih wengine wana dharau na sio wasiri kwani hutangaza majibu na hali za watu.

Watu/makundi mengi yaliyohojiwa yalikiri kutomfahamu wakala wa Tume (RFA) hapo mkoani. Walipoulizwa kuhusu **wakala (RFA)**, walijibu, **“Hatunjui !”**

Ufahamu endelevu pamoja na kampeni za Upimaji wa hiari na Ushauri nasaha , ugawaji mzuri wa kondomu, upatikanaji wa mashine za CD4 mkoa mzima ,ni baadhi tu ya mapendekezo yaliyotolewa na wadau na wenyeji ili kufanikisha kudhibiti maambukizi ya UKIMWI mkoani Kigoma.

Kuna udhaifu mwingi katika upangaji na miundo mbinu inayohitajika kufanikisha mipango hiyo, malalamiko yaliyosikika kutoka takribani kila wahusika wa mkoa ni kuwa mfumo wa kutengeneza na kutekeleza mipango kutoka ‘Juu kwenda Chini’ (TOP-DOWN) inahitaji kuangaliwa upya kwa sababu unakuwa sio shirikishi na huleta matatizo mengi

Katika kuhakikisha kuwa janga la Ukimwi linadhibitiwa mkoani na nchini kwa ujumla, udhaifu wote inabidi utiwe mkazo na kuboreshwa na sekta zingine nazo inabidi ziboreshwe na kupitiwa kila mara ili kuhakikisha UKIMWI unaacha kuwa “JANGA LA TAIFA” .

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Historia.

UKIMWI umetangazwa kuwa janga la kila Mtanzania. Ni hatari kubwa katika maendeleo ya afya ya jamii nzima na mnamo mwaka 2005 kiwango cha maambukizikilikuwa ni asilimia 7. Gonjwa hili la hatari linalopunguza nguvukazi ya nchi linaathiri sana maendeleo ya kiuchumi na jamii.

Kutokana na hitaji la kupitia hali ya Ukimwi nchini, ziara mbalimbali zilifanyika katika baadhi ya mkoa nchini, mkoa wa Kigoma ukiwa mojawapo ya mkoa iliyotembelewa.

▪ Ziara ya Kigoma.

Ziara hii ya wiki moja ilifanyika mwishoni mwa mwezi Oktoba. Washiriki walitoka Wizara ya Afya, Baraza la taifa la watu wanaoishi na Ukimwi (NACOPHA), maofisa na wafanyakazi wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Wakala wa TACAIDS wa Kigoma na Tabora pamoja na wawakilishi na wakuu wa Mkoa, halmashauri na wilaya za Kigoma.

Baada ya kukutana na viongozi na kupokea taarifa ya UKIMWI ya mkoa, timu ilitembelea ofisi za wakala wa Tume na kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za UKIMWI. Kisha baada ya hapo, msafara uligawanyika katika makundi manne yaliyozingatia uwakilishi. Kila kundi lilitembelea Halmashauri husika ambazo ni Manispaa ya Kigoma Ujiji, Halmashauri za wilaya za Kigoma, Kasulu na Kibondo.

▪ Taarifa ya VVU/UKIMWI (2006/2007)

Yafuatayo yalitiliwa mkazo kuhusiana na taarifa hii ya VVU/UKIMWI.

- a. Kondomu nyingi zina matundu madogo ambayo siyo rahisi kuyaona kwa macho, na kati ya kondomu 5, moja tu ndiyo inakua nzima.
- b. Kondomu za kike hazipatikani katika halmashauri ya Kigoma Ujiji na watu hawajui jinsi ya kuzitumia vizuri hizo kondomu.
- c. Kondomu za kiume zilizopo ni chache na zinauzwa.
- d. Ugawaji wa kondomu hauridhishi hasa katika makusanyiko ya watu wengi mfano, katika vituo vya stesheni.
- e. Kuna uhaba wa magari kwa ajili ya kutekeleza shughuli za UKIMWI.
- f. Hakuna ripoti kuhusiana na dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARV), wala idadi ya watu wanaohitaji ARV na wale waliojisajili kwa ajili ya kupata dawa hizo.
- g. Hakuna ripoti kuhusiana na huduma za Nyumbani. (HBC)
- h. Hakuna ripoti inayoelezea idadi kamili ya watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

1.1 Wasaa wa mkoa.

Kutokana na sensa ya mwaka 2002 mkoa wa Kigoma una wakazi wapatao 1,674,047, una wilaya 3, halmashauri 4, tarafa 19, kata 85, vijiji 232 na mitaa 199 (angalia jedwali la utawala hapo chini.)

Jedwali 1: Utawala

WILAYA	TARAFU	KATA	VIJJI	MITAA	VITONGOJI
KIGOMA/UJJI	2	13	0	199	0
KIGOMA VIJJIINI	6	22		0	471
KASULU	7	30	90	0	383
KIBONDO	4	20	67	0	658
JUMLA	19	85	232	199	1,512

Mkoa una eneo la kilomita za mraba 45,075. kati ya hizo, Kigoma ujiji ni 128, Kigoma 19,574, Kasulu 9,315 na Kibondo 16,058.

1.2 Malengo ya Kitaifa katika kudhibiti maambukizi ya virusi vya ukimwi (VVU).

- kupunguza maambukizo mapya ya VVU.
- Kuongeza idadi ya Kiwango cha matibabu ya watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi.
- Kutoa huduma za nyumbani kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi.
- Kuziwezesha familia zilizoathirika pamoja na watu binafsi kurejea katika jamii kwa heshima.

Mkoa unaendelea kufanyia kazi malengo haya ili kuyafikia kwa kusaidiana na wadau walioko mkoani hapa.

1.3 Malengo ya safari.

- Kuangalia na kutathmini hali halisi ya UKIMWI mkoani Kigoma.
- Kukutana na wadau mbali mbali ili kubaini na kupata maoni yao kuhusu hali, vichocheo, yanayotendeka pamoja na ushauri wao kuhusu mwikitio wa kudhibiti UKIMWI.
- Kushauriana kuhusu njia wanazoonza zinafaa kutatua matatizo yanayohusu UKIMWI.
- Kutoa ushauri wa kitaalam unaohusu masuala ya UKIMWI.
- Kuwezesha NACOPHA kuunda Baraza kwenye ngazi ya Halmashauri.

1.4 Mbinu zilizotumika katika kupata taarifa.

- Kutumia maswali ya kuongoza majadiliano (Dodoso).
- Kupitia takwimu/taarifa za mkoa na Halmashauri husika na wakala wa TACAIDS.

- Kukutana na vikundi mbalimbali vikiwemo vya viongozi wa serikali ngazi zote, viongozi wa asasi za jamii, vijana wa kiume, wanawake, wanaume watu wazima, viongozi wa dini, wafanyakazi kutoka nyumba za wageni na baa, walemavu , wanaoishi na virusi vya UKIMWI, wavuvi , wanajeshi, taasisi za elimu, watoto wanaoishi katika mazingira magumu.
- Na kazi nyingine kama ilivyoshauriwa na viongozi wa mkoa na Halmashauri husika.

1.5 Makundi yaliyohusika katika usaili/Majadiliano.

- 5 Kamati ya uendeshaji ya wilaya.
- 6 Wanawake watu wazima.
- 7 Wanaume watu wazima.
- 8 Wasichana.
- 9 Wafanya biashara.
- 10 Vijana wa kiume.
- 11 TTC – chuo cha ualimu.
- 12 Chuo cha uuguzi – nursing school (kabanga).
- 13 Asasi za kiraia.
- 14 WAVIU.
- 15 Walemavu.
- 16 Madhehebu ya dini.
- 17 Vijana wa kiume wenye VVU.
- 18 Wafanyakazi wa kike wa baa, nyumba za kulala wageni na mamalishe.
- 19 Askari.
- 20 Wavuvi.
- 21 Wadau.
- 22 Yatima.

SURA YA PILI

HALI YA VVU/UKIMWI

2.0 Maambukizi ya VVU/UKIMWI.

UKIMWI ni janga la kila Mtanzania. Mkoa wa KIGOMA umekumbwa na janga hilo. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na **TANZANIA HIV/AIDS INDICATOR SURVEY (THIS)** wa mwaka 2003-2004, hali ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI nchini ilikuwa asilimia 7. Maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa mkoa wa Kigoma kutokana na **THIS** ni Asilimia 2.

Kiwango cha maambukizi ya VVU/UKIMWI mkoani mwaka 2005 kilikuwa asilimia 4.65 hali inayoonesha kuongezeka kwa maambukizi mkoani. Mchanganuo wa maambukizi kiwilaya ni kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali 2 (a): Hali ya maambukizi kwa asilimia

WILAYA	MAAMBUKIZI YA MWAKA KWA ASILIMIA	
	2005	2006
Kibondo	5.3%	6.6%
Kasulu	5.9%	6.2%
Kigoma vijijini	4.7%	6.5%
Kigoma/Ujiji manispaa	2.0%	2.3%
JUMLA	4.6%	4.3%

Jedwali 2(b): Taarifa za magonjwa ya ngono mwaka 2006.

UGONJWA	WILAYA	IDADI YA WAGONJWA		JUMLA
		Chini ya miaka 5	Miaka 5+	
GENITAL DISCHARGE	Kibondo	127	1,749	1,876
	Kasulu	293	1,531	1,824
	Kigoma Vijijini	27	858	885
	Kigoma/Ujiji Manispaa	9	553	562
	JUMLA	456	4,691	5,147
GENITAL ULCER	Kibondo	173	1212	1385
	Kasulu	282	687	969
	Kigoma Vijijini	31	275	306
	Kigoma/Ujiji Manispaa	11	140	151
	JUMLA	497	2,314	2,811

PID	Kibondo	137	687	824
	Kasulu	258	1,221	1,479
	Kigoma Vijijini	9	1,008	1,017
	Kigoma/Ujiji Manispaa	25	322	347
	JUMLA	429	3,238	3,667
MAGONJWA YA ZINAA MENGINEYO.	Kibondo	116	1,510	1,626
	Kasulu	278	855	1,133
	Kigoma Vijijini	28	277	305
	Kigoma/Ujiji Manispaa	7	100	107
	JUMLA	429	2,742	3,171

2.1 Ukubwa wa Tatizo.

Imeonekana kwamba tatizo lipo na linazidi kuongezeka kutokana na uwepo wa ongezeko la wagonjwa na vifo na watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Pia kutokana na kuongezeka kwa tabia hatari kama vile masoko mapenzi, mavazi, madanguro n.k.

Washiriki walikiri kupungua kwa nguvu kazi wakati wa shughuli za maendeleo kwa maana ya idadi ya watu wanaoshiriki katika shughuli za maendeleo kupungua kutokana na vifo vya wanajamii na wale wagonjwa ambao hawawezi kushiriki katika shughuli za maendeleo. Hoja hii ilitolewa na mshiriki mmoja na kuungwa mkono na washiriki wote na kufuatiwa na kutaja majina ya watu walioathirika kama kielelezo ili kuonyesha tatizo lilivyo wajumbe walitumia kilinganishi kijozi kama mbinu ya kubaini ukubwa wa tatizo.

Mifano.

- **Kata Mwandiga** – Inaonyesha kuwa katika kaya 10 , nne ni za waathirika, sita ni wazima. Wawakilishi wa kata ya Mwandiga wanakisia kiwango cha maabukizi ni asilimia 40%.
- **Kata ya Mwamgongo** – katika kaya 10 kaya za waathirika ni tano na wazima ni tano , hii nikuonyesha kuwa kiwango cha maambukizi ni asilimia 50% . Sababu zilizotolewa ni kwamba maeneo hayo kulikuwa na kambi ya jeshi, kituo cha polisi na kambi ya wakimbizi. Ina onyesha kuwa kulikuwa na mwingiliano mkubwa kati ya wanakijiji na wageni hasa wanajeshi , polisi na wakimbizi na hivyo kusababisha kuenea kwa maambukizi kwa kasi kubwa.
- **Kata ya Simbo** – katika kaya 10 kaya 3 ni za waathirika na katika zoezi linalo endelea la upimaji wa hiari la kitaifa katika kijiji cha Kasuku kata ya Simbo walipimwa watu 170, waliokutwa na VVU walikuwa 20 hii ni sawa na asilimia 12.
- **Kata ya Mahembe**-katika kijiji cha Mahembe katika kaya 10, kaya nne zina waathirika na kaya mbili zimepoteza wakuu wa kaya na watoto.

2.2 Ufahamu wa VVU/UKIMWI mkoani.

Katika maeneo yaliyo nje kidogo ya mji hali ni tofauti kidogo, watu wengi wanafahamu juu ya UKIMWI na pale kijijini Kalenge(halmashauri ya wilaya ya Kigoma) hawana mgonjwa

wa ukimwi japo kuna dalili nyingi zinazoonyesha kuongezeka kwa hali ya maambukizi na pia kuna ongezeko la tabia hatarishi, kama vile , video za ngono, soko mapenzi, mashine za kusaga kutoa huduma usiku (Kalenge , Mwandiga).

Washiriki wengi katika majadiliano, walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu njia kuu za uambukizi wa UKIMWI na walibaini njia zifuatazo kuwa ni vyanzo vya kuenea kwa ukimwi.

- **Ngono zembe** – katika maeneo wilaya ya Kigoma watu wengi hufanya mapenzi bila kutumia kondomu na hata kama wakitumia hutumia kwa muda tu na kisha kuacha kutumia na tatizo hilo ni kubwa kwa wapenzi wa kipindi kirefu.
- **Kuchangia vitu vyenye ncha kali** – watu wanaendelea na tabia ya kuchangia nyembe na vitu vingine vyenye ncha kali na kwa kufanya hivyo husababisha kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI.
- **Umasikini uliokithiri na ulevi** – familia nyingi zina vipato vidogo sana na wakati mwingine hukosa kabisa kipato cha kujikimu na kulazimika kujiingiza katika ngono kwa ajili ya kupata fedha.

Habari za UKIMWI zinapatikana kupitia:

- ❖ Njia ya redio.
- ❖ Njia ya makongamano /semina.
- ❖ Katika vituo vya tiba.
- ❖ Njia ya TV.

Vilevile kuna makundi yanayojihusisha na masuala ya UKIMWI mkoani Kigoma.

Makundi hayo ni kama vile:

- a. SHIDEPHA+
- b. KIKANGONET.
- c. NDELA
- d. BAPTIST HURU.
- e. KIVIDEA.
- f. BAKWATA
- g. KIMWA.

SURA YA TATU

MATOKEO YA USAILI

3.0 Yaliyopatikana kwenye usaili wa makundi mbalimbali.

■ **Wavuvi (Kijiji cha Mwakizenga Kitongoji cha Muyobozi).**

Kuna mwingiliano mkubwa wa kimapenzi kati ya wageni na wenyeji na kuna tabia nyingi hatarishi zinazoendelea katika kijiji hicho. Masoko ya usiku; kuongezeka kwa nyumba za wageni, biashara ya ngono (kupunguziwa bei ya dagaa/samaki kwa mahusiano ya Ngono)

■ **Wanajeshi.**

Baadhi ya wanajeshi wana mahusiano mapya na askari wenzao hasa baada ya mafunzo ya awali ya kijeshi kukamilika.

Baadhi ya wanajeshi wanajihusisha na mambo ya ngono kwa siri na kumekuwepo na ongezeko kubwa la vifo vinavyo sababishwa na Ukimwi hasa kwa wanandoa. Kwa vijana walio katika mafunzo ya awali kuna tabia ya kubadilishana ngono kwa kusaidiwa kazi za shuruba kama kukata kuni.

■ **Wakuu wa idara.**

Wakuu wa idara za halmashauri walisema tatizo ni kubwa sana, wafanyakazi wengi wanafariki kwa mfano idara ya elimu; katika kipindi cha kuanzia March – September 2007 walimu 12 (3 secondari na 9 shule za msingi) wamefariki. Pamoja na elimu kutolewa walimu wengi hawaamini kuwa wameathirika bali huendelea kuomba ruhusa ili kwenda kwa waganga wa kienyeji.

■ **Wahudumu wa baa wa kike na mamalishe.**

Wanapata manyanyaso na shida nyingi sana, kama vile:

- ❖ Kukosa haki ya kufanya biashara kwa kubugudhiwa na manisipaa. Mfano, mamalishe huishia kukata tamaa na kuingia kwenye biashara ya kujiuza.
- ❖ Matajiri/wamiliki wa mabaa kuchelewa kulipa mishahara pamoja na makato yasiyokuwa na maelezo ya kutosha mfano-kutofika kazini 5000/=, kuchelewa 3,000/=.
- ❖ Uvivu wa wasichana (wakati huohuo wanataka vitu vya thamani) hupelekea wao kujiigiza katika biashara ya ngono.
- ❖ Ulevi wa kupindukia yaani soda, bia na dawa za kulevya kuchanganywa pamoja.
- ❖ Ngono zinafanyika waziwazi kwenye mifereji, viosk na mahali pa giza, na wanaofuatwa zaidi ni wasichana wenye umri chini ya miaka 17.
- ❖ Kumwingilia mwanamke kinyume cha maumbile.

■ **Vijana.**

Tabia/uzoefu wa vijana kuanza ngono mapema imeelezwa kuwa ipo na huanzia umri wa:

- Wasichana: miaka 9 na kuendelea.
- Wavulana: miaka 13 na kuendelea.

Na imeelezwa kuwa;

”Mtoto anapofikisha umri wa miaka 16, huyu huitwa *commando* au *amechaka!*”

Vichocheo vya kuanza ngono mapema imebainishwa kuwa ni:

1. TV zinazoonesha picha za ngono.
2. Tamaa ya kupenda vitu zaidi ya uwezo hivyo huanza tabia ya kuomba fedha kwa wanaume wenye fedha.
3. Tabia ya wazazi kuendelea kulala na watoto wao hadi miaka zaidi ya 7 katika matumizi ya chumba kimoja.

■ **Kamati ya uendeshaji ya wilaya.**

- Halmashauri ina mipango kazi ya UKIMWI na VVU.
- Tatizo la UKIMWI lipo na linaongezeka.
- Tatizo linaongezeka kwa sababu kuu mbili:
 - a. Uandaaji wa mipango na mikakati ni wa mtindo wa kutoka juu kuja chini (top-down style). Kwa mfano kamati za kudhibiti UKIMWI za Halmashauri zimeletwa tu kutoka ngazi za juu kuja kwenye Halmashauri na hazikushirikisha watendaji wa Halmashauri husika.
 - b. Muundo wa kamati za kudhibiti UKIMWI una matatizo. Kwa mfano kutozingatia mchango wa sekta husika na suala la ushirikishwaji kwa ujumla. Mtu asipokuwa diwani hawezi kuwa mshiriki wa kamati ya kudhibiti UKIMWI ya Halmashauri.

3.1 Matatizo yanayowakabili katika maisha yao.

- a. Lishe duni kwa wanaoishi na virusi.
- b. Kubaguliwa na kutengwa na jamii kwa wanaoishi na virusi.
- c. Ukosefu wa elimu ya matumizi sahihi ya kondomu, hutumia mifuko ya Rambo badala ya kondomu kwa kujikinga na maambukizi ya virusi vya Ukimwi.
- d. Kunyanyapaliwa kwa wanaoishi na virusi vya Ukimwi.
- e. Ukosefu wa elimu Stadi za maisha.
- f. Umaskini unaopelekea baadhi ya wazazi kuwatumia watoto wa kike kama chanzo cha kupata fedha.
- g. Kutokuwepo sheria ndogondogo zilizowekwa hapa mkoani ili kudhibiti maambukizi ya virusi vya ukimwi, mfano:

”Wasiendeleo kunywa hadi usiku mrefu ,inasababisha watu kubakwa wakati wa usiku!”

3.2 Njia kuu za maambukizi.

Njia kuu za maambukizi zilizobainishwa na makundi mbalimbali ni:

1. Ngono zembe.

2. Kuchangia vitu vyenye ncha kali kama sindano, nyembe n.k.
3. Kuongezewa damu yenye virusi vya Ukimwi.
4. Mtoto kupata virusi vya Ukimwi kutoka kwa mama yake.

3.3 Vichochezi vya maambukizi.

- Majumba ya video.
- Picha chafu za ngono.
- Majumba ya disco yanayofanyika mara tatu kwa wiki na mpaka saa 11 asubuhi
- Kipato kidogo kwa wanafamilia inayopelekea biashara ya ngono inayofanyika wakati fulani kwa shilingi 500 mpaka 1000 bila kondom kulingana na dau analotaja mteja. Sababu kubwa ni uvivu wa wanaume kutokuwajibika na kushinda kwenye michezo kama vile pool, draft, kwenye baa na vilabu vya pombe za asili.
- Sehemu za burudani ni nyingi ambazo mara nyingi zinakosa kondom.
- Pombe kuu vilabuni inanywewa toka saa 12 asubuhi na inapofika jioni wanafanya ngono hadharani bila kondom.

“Mimi niliwahi kushuhudia ngono hadharani na tukawafukuza wahusika”

- Wamiliki wa vilabu vya pombe zisizo rasmi huendesha biashara ya vyumba kwa ajili ya ngono.
- Watumishi wa mashirika ya kimataifa wana fedha nyingi na zinatumika kununulia ngono.
- Kutetereka kwa ndoa: Wanaume huwa wana nyumba ndogo. Wanawake nao huenda kutafuta wapenzi nje ya ndoa ili kulipa kisas.i
- Mila: watu wengi wameacha mila zinazozuia maambukizi. Watoto hawadhibitiwi tena na huachwa kufanya lolote wanalotaka.
- Kundi la waathirika wanawake walibaini chanzo kimoja wapo ni kuuguza wagonjwa bila kuchukua tahadhari.
- Ujio wa wakimbizi hususani waishio nje ya makambi umeathiri mila na desturi za watanania wa maeneo haya . Wakimbizi wengi wamekuwa na tabia ya ulevi wa kupindukia na kushawishi vijana wengi wa maeneo haya kuiga tabia hii mbaya , tabia ya ulevi iliyoletwa na wakimbizi imewafanya vijana kujiunga katika makundi ya ulevi ambayo huambatana na ngono zembe.
- Wanaume wengi huona fahari kuoa binti aliyezaa kwa vile huamini kuwa amejifunza ugumu wa maisha na akiingia kwenye ndoa atadumu na pia ana uwezo wa kuzaa, hali hii huchochea wasichana kuanza mapenzi wakiwa wadogo na yasiyo salama na kuwaweka katika hali ya kupata uambukizo wa UKIMWI.
- Tabia ya kufunga ndoa bila kupima huchangia kuenea kwa maambukizi mapya.
- Kukosekana kwa sheria ndogo ndogo katika ngazi ya kitongojji katika kudhibiti mienendo ya shuguli za usiku kama vile ; Soko mapenzi(masoko ya usiku), mashine za kusaga unga usiku tu.
- Madisco ya usiku na katika sherehe za usiku.
- Matangazo ya redio kama vile; usiku wa mahaba, michezo ya kuigiza ya TV na Redio.

- Vijana na wavuvi walisema kukosekana kwa shughuli maalumu huchochea vijana kujiingiza katika mahusiano ya ngono.
- Vijana wameanza kuangalia kanda za video ambazo zinaonyesha ngono. Baada ya kuangalia kanda hizo, vijana wanakwenda kufanya majaribio.
- Soko la jioni limechangia wana kijiji, Wake kwa Waume kukaa hapo mpaka usiku.
- Nyumba za kulala wageni zilizojengwa vijijini zimeanza kutumika kwa kufanya ngono.
- Disco la usiku katika sherehe mbalimbali kama harusi, krismasi, IDDI Mubarak n.k

3.4 Maoni/Mapendekezo.

Kamati ya Uendeshaji ya wilaya.

Maoni.

- Rasilimali zinazokuja kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI bado ziko katika mtindo wa kutoka juu kuja chini (top-down style) yaani mipango inapangwa kutoka ngazi za juu na kuhitajiwa kutekelezwa katika ngazi za chini. Michango ya sekta mbalimbali haizingatiwi kama vile sekta ya kilimo, utamaduni, elimu n.k. haifuatwi kama sio kutozingatiwa.
- Kutotolewa kwa fursa za elimu ya UKIMWI kwa watumishi wa chini wa sekta mbalimbali
- Kuhusu maambukizi ya UKIMWI kwa Kasulu imeonekana watu wa mjini wana uelewa mkubwa zaidi ya watu wa vijijini.
- Hakuna huduma rafiki za vijana.
- Sheria: Zote ziangaliwe upya hasa zile ambazo zinachangia maambukizi ya UKIMWI kwa mfano sheria za ndoa, mirathi n.k. Sheria hizo zipewe meno.
- Mchango wa asasi: Imeonekana wakati fulani kuna asasi ambazo huja Wilayani kufanya kazi maeneo ya Halmashauri bila kushirikisha mamlaka zinazohusika na kusababisha mgongano kwa mfano kufanya afua zinazofanywa na asasi au taasisi zilizopo.
- Matumizi ya kondom hayajaeleweka. Bado kuna tafsiri potofu kama vile kwamba kondom zina vitundu vidogo vinavyopitisha virusi vya UKIMWI na kwamba wazungu wanataka kutumaliza wote.
- GFS code ya rasilimali za UKIMWI: rasilimali zote ni lazima ziingie kwenye GFS code ya serikali kama ilivyo kwa MTEF.
- Jinsi elimu inavyotolewa: Wahamasishaji wanapohamasisha hasa katika maeneo ya mijini elimu hiyo haitandazwi hadi sehemu za vijijini kama vile ISHI campaign.
- Suala la UKIMWI NA VVU halimo kwa kina katika mitaala ya elimu.
- Taasisi za dini zihusishwe katika suala la UKIMWI NA VVU kwa kuwa viongozi wa dini wanasaidia sana katika kupunguza mmomonyoko wa maadili na ya kuwa wenye stadi hizi ni wachache.
- Suala la viongozi wa dini liangaliwe upya hasa ukizingatia kwamba madhehebu ya dini ni mengi kila moja likiwa na imani zake.

Wanawake (watu wazima).

- Kuongeza kipato cha wakina mama. Serikali iwaandalie mazingira ya ajira kwa mfano elimu ya ujasiriamali
- Wanahitaji kuwa na mwongozo wa uongozi/uendes haji wa vikundi vya wakinamama
- Mahali pengine wameona mashirika hasa Red Cross na TARUDEREO wakitoa elimu ya UKIMWI.
- Watu hawajitokezi kupima kwa hiari kwa sababu ya kukosa usiri.
- Huduma za majumbani zinatolewa kwa waliojiandikisha tu, waangaliwe pia na wale ambao hawajajiandikisha.

Wanaume (watu wazima)

- Ziundwe kamati/vikundi vya kijamii vinavyoshughuhulisha na masuala ya UKIMWI na VVU kuanzia nyumba hadi nyumba na viwe vinafanya kazi.
- Sheria ndogo ndogo ziimarishwe kudhibiti janga: hasa kuhusu picha chafu, baa, nyumba za kulala wageni n.k.
- Pale inapotokea vifo, kitajwe chanzo cha kifo na sio kusingizia maradhi mengine kama malaria na typhoid.

Wafanyabiashara.

Maoni:

- Maambukizi ni makubwa sana karibu na soko.
- Usambazaji wa UKIMWI wa makusudi: Kwa mfano soko mapenzi – linaloanza saa 1.30 usiku, baa, vilabu kama Msundule (mwanamke avuliwe nguo).
- Nyumba za wageni bubu – Migombani na Kibangwe huchangia kuenea kwa UKIMWI.

Mapendekezo:


- Elimu ya UKIMWI ianzie katika umri mdogo.
- Elimu itolewe kwa wafanya biashara.
- Serikali iendeele kuwakusanya vijana na kutoa elimu.
- Serikali izuie baa kufunguliwa asubuhi.
- Serikali ihamasishe kilimo lakini izingatie kuwa walaji ni wengi. Kwa mfano Mzee Yusuf Makamba alisimamia vizuri suala hili.
- Wasiofanya kazi hawachukuliwi hatua zozote, inabidi wasaidiwe.
- Serikali isichoke kuhamasisha kupima.
- Mtu akifa na tatizo la UKIMWI atangazwe.
- Kupima iwe lazima kwa kila mtu anayehudhuria kituo cha tiba kwa huduma yoyote.

“Kutoa majibu ya uongo hasa kwa wale wanaobainika wana maambukizi hasa wakati wa kutaka kuoana ipigwe vita”

- Kuna umuhimu wa jamii kuwa wazi ndugu anapofariki kwa UKIMWI.

Vijana.

- Kuwawezesha vijana kupata stadi za maisha
- Vituo vya vijana viongezwe.
- Viongozi wa madhehebu, wawe mifano bora.
- Elimu kuhusu UKIMWI itolewe kwa wingi, kupitia vyombo vya habari, kama vile vipindi maalum radioni.
- Vikundi vya kuhamasisha havitoshi, viongezwe.
- Semina za kuhamasisha kupiga vita UKIMWI zifanyike vijijini kwa watu wote.



Tujenge desturi ya kujisomea

- Kuwe na maonesho ya wazi kwenye majukwaa ya kuzuia VVU. Mabango yawepo mitaani na yafike hata vijijini ambako hivi sasa hayapo.
- Vikundi vya wahamasishaji vya sanaa vifanye uhamasishaji mjini na vijijini ili watu wapime. Hii itasaidia kuondoa dhana potovu mfano kuvaa kondom.
- Msaada kwa yatima uongezwe kwani wengi hawajafikiwa na maisha duni yanachangia kurubuniwa.
- Pamoja na ushauri kuanza kupima mapema pia walisema kuwa wanawake wanao patikana kuwa wana maambukizo, wapate ushauri sahihi kuhusu uzazi.
- Itengenezwe sheria juu ya mavazi ya wasichana ya kubana, vijana kuhusu madawa ya kulevya na nyumba za wageni zinazotumika kama mahala pa ngono, madanguro ambayo yanazidi kufunguliwa (Kibondo).
- Kuepuka sababu zinazompelekea mtu kuhitaji kuongezewa damu na kuelimisha wanawake wote wazalie kwenye huduma za afya.
- Upatikanaji wa kondom kwa vijana ulionekana kuwa sio tatizo, lakini vijijini hazifiki.

Chuo cha Ualimu (TTC)

- Kupima afya iwe ni lazima.

- Waathirika watangazwe hadharani.
- Matangazo ya TV yatangaze kuzuia ngono badala ya kuchochea ngono.
- Sheria za chuo kuhusu ngono ziondolewe hasa kutotakiwa kuwa na kondom.
- Watumishi wa idara ya afya hawawi wazi iwapo mtu amekufa kwa UKIMWI.

Chuo cha Uguzi Kabanga.

- Mtaala wa UKIMWI uwekwe katika mafunzo na kwa undani.
- Sheria na sera zirekebishwe.
- Washirikishwe katika kutengeneza mipango na mikakati ya kudhibiti UKIMWI.
- Hospitali kutokuwa na vifaa vya kutosha vya kukinga maambukizi kama vile gloves, izingatiwe na serikali.
- Msimamo wa kanisa katoliki wa kutoruhusu matumizi ya kondom lazima uzingatiwe.

Asasi za kiraia.

Maoni:

- Kuna watu wengi ambao hawafanyi kazi na hawajishughulishi na kazi yoyote; Kuwe na mkakati wa makusudi kufundisha ujasiriamali.
- Ucheleweshaji wa fedha na utaratibu mzima wa kupokea na kutoa fedha kwa ajili ya mradi unakwamisha harakati za kupambana na UKIMWI.
- Kampeni ya kupima kwa hiari isiwe ya muda mfupi lakini iendelezwe kwa vipindi vya mara kwa mara.
- Mratibu wa sasa wa UKIMWI ana majukumu mengi hivyo ni vigumu kuweza kushughulikia kikamilifu masuala ya UKIMWI katika Wilaya. Yeye ni mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii, mratibu wa maboresho ya sekta pia.
- Uwakilishi wao kwenye CMAC hautoshelezi na upatikanaji wake haukuwa shirikishi.
- Mtandao wa asasi ni dhaifu na wameshauri kuufufua.
- Hakuna mkakati wa uendeleu na wameshauri ufanyiwe kazi.
- Kuimarisha ushirikiano kati ya wana-asasi na Halmashauri ili kushirikiana badala ya kutofautiana. (Kuelewana na sio kuzozana)

Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU).

- WAVIU walipendekeza kuwa:

“Wale ambao bado hawajaambukizwa watumie kondom kwa wakati wote na wale ambao tumeambukizwa, pia tutumie kondom ili tusiwaambukize wengine”.

- Mapendekezo yao mengine yalilenga kwenye kuongeza elimu ya kinga ya vijana wa sekondari na primary. Elimu hiyo waliona ni bora ianze mapema kwa vile kwa maoni yao ngono inaanza baina ya miaka tisa na kumi.
- Uelimishaji wa wanaoishi na UKIMWI uendele.

- Wanaoishi na virusi vya UKIMWI wawe wazi kuhusu maambukizi waliyokuwa nayo hasa kwa familia zao.

“WAVIU wasipewe *septrin* tu bali tuwe tunaanzishiwa dawa mume na mke, kwani akianzishiwa mke peke yake sitaruhusiwa kufanya naye tendo la ndoa”.

- Waliomba kuwe na mashine ya kupima CD4.
- Kwa vile katika kundi hili wengi ni wakulima, wengi wao wakiwa bado wana nguvu serikali iwafikirie kuwasaidia kwa kuwapa mbegu na pembejeo/zana, pia wafikiriwe msaada wa miradi midogomidogo itakayowawezesha kupata kipato.
- Walipendekeza kupewa msaada wa chakula hasa wiki za mwanzo wanapoanzishiwa dawa.
- Kuwe na uwazi zaidi kwa huduma na misaada inayotolewa kwa WAVIU.
- Serikali itunge sheria ya kuzuia unyanyapaa.
- Mafunzo yatolewe kuwezesha WAVIU waliojiweka wazi – kujitangaza hadharani, kuweza kuishi na jamii.
- Sheria ndogondogo zitumike/zitungwe kudhibiti mikesha na sinema za usiku zikiwemo sinema za ngono.

Walemavu.

Maoni:

- UKIMWI unaathiri sana. Unaathiri nguvu kazi na unaongeza vifo.
- Hatujawahi kuhudhuria mipango ya kudhibiti UKIMWI.
- Habari za UKIMWI tunapata mitaani kwenye redio tu.

“Sijawahi kupata elimu ya kutumia kondom hivyo situmii hata nikienda nje”

“Sitoki nje ya ndoa”

- Walemavu hawathaminiki afadhali ya malaya.
- Kuna walemavu wanauza ngono kwa sababu ya shida kwa viwango vya kuanzia sh. 500 – 1000 na wengine kwa sahani ya wali tu. Na hasa kama ana mtoto mdogo hufanya hivyo ili apate chakula cha mtoto.



Watu wenye ulemavu wanahitaji kuingwa na maambukizi ya UKIMWI

“Kuna kipindi cherehani yangu ilivunjika. Inabidi upite vilabuni kupata machicha. Nafanya mapenzi ili watoto wangu wale. Hapo nilikuwa na mshono”

“Walemavu hatuna shamba wala kazi”

- Wapo walemavu ambao ndoa zao sio salama. Wana nyumba ndogo. Wanawake wanalipiza kisasi.
- Hatuna forum/ofisi ya chama chetu kinachoitwa CHAWATA tawi la Kasulu. Hatuna mawasiliano na CHAWATA taifa.

Wakala wa Tume ya kudhibiti UKIMWI wa mkoa: “Hatunjui”

Ushauri:

- Wengine wameathirika, wapewe msaada wa kutosha.
- Ni muhimu kuwa na mwakilishi wetu katika kamati za kudhibiti UKIMWI.
- Tuwezeshwe ili tujikimu na maisha kama vile kwa mikopo midogo midogo na kila mtu abuni mradi wake.

“Lakini ukiugua nyumbani sina fedha ya kutibiwa mpaka nachimba miti shamba ili nipone. Hospitali mpaka niwe na hela za cheti na matibabu yananishinda. Tunaomba kutibiwa bure”

Viongozi wa dini.

- Tunasisitiza watu waepuke zinaa.
- Ikishindikana kwa msichana kupata kipato tueleze viongozi wa dini tujaribu kumsaidia; tumewasaidia wengi.
- Pamoja na mihadhara misikitini watu hawajabadili tabia.
- Tusichoke kuhubiri.

“Wake wengi inategemea na tabia ya mtu. Inawezekana kuwa na mke mmoja na usitoke nje na ukawa na wengi ukatoka nje ya ndoa hizo”

Kuhusu wakala wa Tume yaani RFA: “Hatunjui”

Ushauri:

- Tuendeleo kuhamasisha na kuwaonya watu waache zinaa.
- Kupima mara kwa mara kuona kama afya yako ni salama.
- Kuepuka njia zote zingine za maambukizi.
- Jamii ihamasishwe kwenda kupima kwa hiari.
- Viongozi wafanye vitendo badala ya kuongea tu bila kufanya lolote.
- Lazima kuwe na sheria inayozuia baa na nyumba za kulala wageni kutumika kama sehemu za kufanya biashara ya ngono.
- Vifo vinavyotokana na UKIMWI vitangazwe hadharani badala ya kuficha ukweli ili kujenga hofu miongoni mwa wanajamii juu ya UKIMWI.

Vijana wa kiume wanaoishi na Ukimwi.

Ushauri:

- Elimu ya UKIMWI izidi kutolewa.
- Zoezi la upimaji liendeleo mara kwa mara.
- Upimaji pia usogezwe karibu na wananchi (uchache wa vituo vya upimaji.)
- Kupewa misaada ya kiuchumi.

“Kama watu wakipewa misaada watu zaidi watajitokeza”

- Kuanzisha vikundi vya waathirika kutiliwe mkazo.

3.5 Nini kifanyike kupunguza maambukizi.

- Akinamama wawezeshwe mitaji na mafunzo ya ujasiria mali. Miradi iliyopendekezwa ni bustani, ulimaji wa miwa na ufunguzi wa migahawa.
- Wasichana na wavulana walipendekeza kuwa waepukane na mambo ya disco, na vilabu vya pombe.
- Vijana waelimishwe zaidi kuhusu masuala ya Ukimwi na wawe wawazi baada ya kupima, pia wabadilishe tabia baada ya kupima nakujitambua kuwa wameathirika au la.
- Elimu itolewe mara kwa mara kwa vijana na jamii kwa ujumla.
- Wataalam wafike mara kwa mara ili kuelimisha jamii.
- Mashindano ya urembo yasifanywe rasimi na serikali isijihusishe nayo.
- Watoto wa kike wasitumike kunengua katika maonyesho ya biashara.
- Selikali ianzishe na kuimarisha ‘Mobile VCT’ kwa vile watoa huduma wageni huaminika zaidi katika usiri.
- Watu mashuhuri wa vijijini wapewe mafunzo na wawezeshwe katika kutoa elimu ya UKIMWI kwa vile wao husikilizwa zaidi na jamii.
- Watu wanaoishi na virusi vya ukimwi wawezeshwe ili waweze kupata uwezo wa kujihudumia wenyewe.
- Kuwa waaminifu katika ndoa ni muhimu.
- Elimu ya ukimwi itolewe mashuleni katika kiwango cha kujikinga na kuacha ngono.



Utashi wa kisiasa ni hatua muhimu katika kuukabili UKIMWI

3.6 Vikwazo vya kupima UKIMWI.

- a) Umbali kutoka kijijini hadi sehemu ya kupimia.
- b) Kutokuwepo kwa huduma ya ushauri nasaha na kupima.
- c) Akinamama wapo tayari kupima ila akina baba hawapo tayari.
- d) Hofu ya kupima kwa sababu akikutwa yeye ana virusi vya UKIMWI anaogopa kunyanyapaliwa na jamii.
- e) Wahudumu wa upimaji na ushauri nasaha ni wachache sana ukilinganisha na huduma inavyo hitajika. Na washauri nasaha waliokaa muda mrefu kituo kimoja wahamishwe ili kuongeza ufanisi na usiri.
- f) Vituo vilivyopo viwe na utaratibu wa utoaji wa huduma unao jitosheleza , mfano imejitokeza watu hupimwa katika kituo cha Angaza na kuelekezwa waende katika hospitali ya Maweni kwa huduma zaidi ya upimaji wa CD4.
- g) Baadhi ya zahanati hazina huduma ya ushauri nasaha na upimaji hivyo wapelekewe washauri nasaha na vifaa vya kupimia ili huduma hii iwafikie watu walio wengi.
- h) Elimu ya UKIMWI itolewe kuanzia ngazi ya kitongoji pia kwa viongozi wa madhehebu mbalimbali ili wawaelimishe waumini wao.
- i) Elimu ya UKIMWI itolewe kwa wengi badala yawachache vijijini.
- j) Wavuvi walishauri wapatiwe elimu zaidi juu ya ngono salama.
- k) Ushirikiano na jamii ni muhimu sana.
- l) Hali ya unyanya paa ni kubwa sana katika jamii hii ya kigoma , wagonjwa wanatengwa sana , wahudumu wa afya mara nyingi wameitiwa wagonjwa walioko majumbani ili kuwahudumia.

Ili kushinda na kuepukana na vikwazo vilivyoorodheshwa, inabidi udhaifu wowote unaojitokeza urekebishwe katika kila sekta.

3.7 Madhara yanayotokana na Ukimwi :

- a. Kuwepo na watoto yatima.
- b. Kuwepo na wagare na wajane.
- c. Watoto kuishi maisha magumu yanayopelekea kuwa ombaomba, wezi, ubakaji, utumiaji wa madawa ya kulevya.
- d. Uchumi wa familia hupungua kwa kutumia muda mwingi pamoja na fedha kumhudumia mgonjwa wa Ukimwi.
- e. Unyanyapaa kwenye biashara, mfano mama ntilie wauza vitumbua, wauza daga hukosa/ hukimbiwa na wateja.

SURA YA NNE

URATIBU KATIKA MKOA

4.0 Uratibu katika ngazi ya mkoa.

Kwa ujumla uratibu wa shughuli za UKIMWI upo na unafanyika, kwa mfano Idara za Elimu, Kilimo na Maliasili watashirikiana na Wizara ya Afya (DACC) katika kutoa elimu ya UKIMWI na magonjwa ya zinaa kwa wafanyakazi wao. Ushirikishwaji wa wafanyakazi hawa wawili ni kwa usawa na kwa pamoja na imeonekana mmoja alipokuwa mafunzoni kazi za DACC alimwachia CHAC.

Mfano mwingine ulitolewa na Mhandisi wa Maji ambaye anashirikiana na DACC akienda kwenye shughuli za “field” anapatiwa vitendea kazi kwa mfano kondom, vipeperushi vya kuelimisha wafanyakazi wa barabara.

Kuna Uwepo wa uratibu wa shughuli za wadau kutoka Asasi mbalimbali. Uratibu wa Asasi za kiraia unafanywa na Halmashauri kwa Asasi kuwajibika kwa Halmashauri kwa kuleta taarifa za utekelezaji wa shughuli za UKIMWI na pia asasi hizo zote zimejisajili na zinafahamika kwenye Halmashauri.

Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kwenye wilaya (CMACs) inaratibu na kusimamia shughuli zote za asasi za kiraia zinazojihusisha na mapambano ya UKIMWI kwenye halmashauri yao.

Huduma za UNV zilianza Oktoba 2006. Kazi kubwa ya UNV ni kukuza mwitikio wa jamii katika mapambano ya UKIMWI kwa kujenga uwezo wa jamii katika kutambua, kupanga na kutekeleza mipango ya vijiji/mitaa. Mipango hiyo inategemea rasilimali walizonazo wanajamii. Aidha mipango hiyo ni chanzo cha kupata mpango mkakati (Council Comprehensive Plan – CCP).

Aidha, Idara ya Mipango ya Halmashauri inaratibu na kusimamia usambazaji wa taarifa za UKIMWI kwa wadau mbalimbali ikiwemo Kamati za Kudumu za Halmashauri.

Uratibu katika ngazi ya mkoa unategemea sana uratibu unaofanyika katika wilaya.

▪ Uratibu katika ngazi ya wilaya

Katika ngazi ya wilaya uratibu upo, kamati za UKIMWI zimeundwa katika kila halmashauri na vikao vinakaa kila baada ya miezi mitatu. Pia kamati hizo zote zina mipango ya utekelezaji. Kamati za UKIMWI za kata na Vijiji/mitaa zimeundwa na baadhi zimefundishwa lakini nyingi hazikutani na wala hazijajengewa uwezo ili kutekeleza majukumu yao.

Asasi zote zilizopo kwenye Halmashauri zinatambulika na zinawajibika kwa Halmashauri. Aidha mkoa na Halmashauri unashirikishwa katika kuzitambua na kuhakiki mipango yao kwa kushirikiana na wakala wa TACAIDS.

Mkoa una mtandao wa asasi za kiraia zinazoshughulika na UKIMWI ambapo kila wilaya ina uongozi wake.

Ushirikishwaji wa Mipango ya Kudhibiti UKIMWI katika Halmashauri bado siyo shirikishi kwa kuwa upatikanaji wa fedha ni kidogo na ushirikishwaji wa kamati za UKIMWI za Kata na Vijiji /mitaa bado ni mdogo.

■ **Kamati ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Mkoa.**

Kamati hii kupitia Mratibu wa kudhibiti UKIMWI wa mkoa (RACC) inasimamia uratibu wa huduma hizi kupitia Mratibu wa kudhibiti UKIMWI wa Wilaya (DACC) katika kusaidia kuandaa mipango, kujumuisha mahitaji ya dawa na vifaa, tiba kwa ajili ya UKIMWI na kupeleka taarifa ngazi ya taifa.

4.1 Idara za halmashauri.

Inaonekana kwamba baadhi ya idara katika Halmashauri ndizo zina mipango ya kudhibiti UKIMWI sehemu za kazi. Aidha Manispaa ya Kigoma Ujiji ina mpango maalum wa kudhibiti UKIMWI mahali pa kazi.

Idara zilizokuwa hazijaanza zilikiri kuona umuhimu wa kuwa na mpango wa UKIMWI kwa wafanyakazi lakini bado hawajaanza kutokana na kutopata msukumo wa kutosha na woga wa kuwa na bajeti finyu, na kutoelewa kazi zinazoweza kutekelezwa.

Baada ya majadiliano waliahidi kutayarisha mipango inayojumuisha sekta zote.

Mipango ya halmashauri.

i) Mpango wa 2006/2007

Kipaumbele cha mwaka 2006/07 kilikuwa kuimarisha huduma za ushauri nasaha na kupima afya. Lengo lilikuwa ni kuongeza vituo vitatu (2006) kufikia kumi na moja (2007). Vituo vimefikia vitano hadi mwezi (Oktoba) kazi ya ukarabati wa vituo sita vilivyobaki inaendelea.

Kazi hii ilitumia karibu robo tatu ya bajeti nzima ya fedha kutoka Global Fund.

Kazi nyingine za kawaida ikiwemo kinga, kuelimisha umma na tiba ziliendelea kama kawaida.

Halmashauri ilikuwa na mpango wa kupanua utoaji wa huduma za tiba kwa WAVIU kutoka kimoja (2006) kufikia vitatu (2007). Katika kufanikisha hilo halmashauri inafanya kazi kwa karibu na mitandao ya WAVIU katika uhamasishaji wa jamii.

ii) **Mengineyo.**

- Kuimarisha kamati ya kudhibiti UKIMWI mahali pa kazi.
- Kuimarisha vikao vya wakuu wa idara vya UKIMWI vya kila mwezi.
- Kuimarisha vikao vya kila mwezi vya maafisa ugani na kuleta taarifa kila mwezi.
- Kuendesha semina za UKIMWI kwa madiwani na wadau mbalimbali.

4.2 **Idara za afya.**

Idara ya Afya katika Halamashauri zote za mkoa wa Kigoma zilizotembelewa imeonekana zinafanya uratibu na kutoa huduma kama inavyotakiwa. Aidha huduma za UKIMWI zinazotolewa ni kama zifuatazo:-

- Ushauri Nasaha na Kupima virusi vya UKIMWI.
- Huduma ya damu salama (Kupitia kanda ya Tabora).
- Elimu ya kujikinga na UKIMWI zikiwemo njia za vipeperushi na vipindi vya redio.
- Matibabu ya magonjwa ya ngono.
- Huduma ya kuzuia maambukizo ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT).
- Utoaji wa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARVs).
- Kutoa huduma za wagonjwa majumbani (HBC).
- Kujenga uwezo wa watumishi kwa kuwapa mafunzo rejea ya utoaji huduma kwenye maeneo husika kama vile VCT, ARV, PMTCT, HBC na zingine nyingi.
- Huduma rafiki kwa vijana (kibondo na Manispaa ya Kigoma Ujiji).

1) **Mafanikio.**

Mafanikio ya sekta ya Afya/Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni kwamba huduma zimeboreka na kumekuwa na ongezeko la wagonjwa ambao wanapata dawa katika ngazi zote katika vituo vyote vya serikali na vya mashirika binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali na ya dini . Aidha mfumo wa huduma za wagonjwa majumbani, kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto nazo zimeboreshwa.

2) Matatizo.

- i) Huduma za Kinga bado ni dhaifu hasa katika utoaji, usambazaji na matumizi ya kondom. Pia imeonekana kuna imani potofu kuhusiana na matumizi na ubora wa kondom.
- ii) Ukosefu au udhaifu wa miundo mbinu inayoendana na utoaji wa huduma za udhibiti wa UKIMWI.
- iii) Ukosefu wa mashine za CD4 kwenye hospitali ya wilaya ya Kibondo na ubovu wa CD4 mashine ya hospitali ya wilaya ya Kasulu.
- iv) Kuna upungufu wa magari kwa ajili ya kuendesha huduma za afya.

4.3 Usambazaji wa kondomu.

- ❖ Kondomu zinapatikana na zipo, zinapatikana kwa kuuzwa (Kigoma Ujiji) na katika zahanati.
- ❖ Kondomu zinapatikana zahanati na maduka ya madawa hata hivyo hawapendi kuchukua zahanati kwa hofu kuwa wataonekana ni wazinifu.
- ❖ Hazitumiki sana kwa wenyeji, zinatumiwa kwa wageni, watu ambao hawajajulikana katika maeneo husika.
- ❖ Zinanunuliwa kwa uficho.
- ❖ Katika kipindi cha Januari – Septemba 2007, idadi ya kondomu zilizosambazwa ni 1,656,000.

4.4 Huduma ya upimaji wa Hiari na Ushauri Nasaha.

Utoaji wa huduma ya upimaji wa hiari na ushauri nasaha una endelea kufanyika Mkoani kupitia vituo 26 kwa mwaka 2006 vya kutolea huduma hiyo ambapo Manispaa ina vituo 6, Kibondo vituo 4, Kasulu vituo 6 na Kigoma Vijijini vituo 10. Vituo vyote hivyo vilikuwa na wanasahi wapatao 98 mwaka 2005 na 102 mwaka 2006 ambapo mwaka huu wengi wanaendelea kupata mafunzo katika wilaya zote.

Jedwali Na. 4(a): Ushauri nasaha na upimaji wa hiari (VCT), 2005

Wilaya	Idadi ya vituo vya VCT	Idadi waliopimwa (Jumla)	Walioambukizwa	
			Idadi	Asilimia (%)
Kibondo	4	2,130	113	5.3%
Kasulu	4	3,019	180	5.9%
Kigoma Vijijini	3	1,868	88	4.7%
Kigoma/Ujiji Manispaa	3	2,133	44	2.0%
JUMLA	14	9,150	425	4.6%

Jedwali Na. 4(b): Ushauri nasaha na upimaji wa hiari (VCT), 2006

Wilaya	Idadi ya vituo vya VCT	Idadi waliopimwa (Jumla)	Walioambukizwa	
			Idadi	Asilimia (%)
Kibondo	4	1,490	98	6.6%
Kasulu	6	1,905	119	6.2%
Kigoma Vijijini	10	1,182	77	6.5%
Kigoma/Ujiji Manispaa	6	1,630	36	2.3%
JUMLA	26	6,207	330	4.3%

▪ **Kampeni ya Ushauri Nasaha na Upimaji wa Hiari.**

Baada ya Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuzindua Kampeni ya ushauri nasaha na upimaji wa hiari tarehe 14/07/2007, mkoa wa Kigoma haukubaki nyuma.

